BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Tisa – Tarehe 01 Oktoba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018.

Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Ripoti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018.

Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi na Mawasiliano:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano Kuhusu Ripoti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018.

III. MASWALI:

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

05. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa muda mrefu sasa bwawa la maji la Sebleni limekuwa kero kwa wakaazi wa jirani na bwawa hilo kila kipindi cha mvua ndogo na kubwa, kutokana na kujaa maji na linaonekana kama limeshashindikana kutafutiwa ufumbuzi.

(a) Je, kuna mpango gani wa kulijenga bwawa hilo.

(b) Je, kuna mpango wa kuwahamisha wananchi wanaoishi kando ya bwawa hilo.

(c) Je, Serikali imajipangaje kuwalipa fidia stahiki wananchi watakaoathirika na mpango huo kabla ya kuwaondoa.

Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:

93. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Tarehe 15/07/2018, vyombo vya Habari vya Serikali vimeripoti hatua za uongozi wa Ofisi ya Mufti kutembelea kisiwa cha Tumbatu ili kufanya suluhu ya mgogoro unaodaiwa kusababishwa na mambo ya kisiasa ambapo inadaiwa kuwa watu hawazikani na wanasusiana shughuli za kijamii.

(a) Je, Ofisi ya Mufti imebaini mgogoro huo upo kwa muda gani.

(b) Je, hatua gani za ziada zimechukuliwa kuondoa mgogoro huo.

(c) Je, Serikali haioni ulazima wa kuja na mkakati wa kudumu wa kuondoa matatizo hayo.

97. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Sheria ya Mawakili wa Kujitegemea Sura ya 28 ni sheria ya miaka mingi tokea wakati wa ukoloni mpaka hivi sasa na haijafanyiwa marekebisho licha ya mabadiliko kadhaa yaliyojiotekeza katika fani hiyo ya Uwakili hapa nchini.

(a) Je, lini Serikali itaileta Sheria hiyo Baraza la Wawakilishi kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho au kutungwa upya ikilazimu.

(b) Hatua gani zimechukuliwa kuipitia Sheria hiyo kwa ajili ya kufanyiwa marekebisho au kuandikwa upya.

(c) Kuendelea kutumia Sheria hiyo inayoonekena kupitwa na wakati, Je, Serikali haioni kuwa inarudisha nyuma maendeleo ya upatikanaji haki kwa vile Mawakili wa Kujitegemea wanafanya kazi kubwa kuisadia Mahakama kufikia uamuzi wa haki.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

123. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Katika miaka ya nyuma, wanafunzi maskulini walikuwa wakifundishwa kazi za mkono, kilimo, ufugaji na kadhalika na hivyo kuweza kujiajiri wenyewe wanapomaliza masomo yao jambo ambalo kwa kiasi kikubwa limeondoka na kusababisha wahitimu wengi kusubiri kuajiriwa tu.

(a) Je, Serikali imeondoa mtindo ule wa ujasiriamali kuonekana haufai.

(b) Je, Serikali haioni kuwa inapata kazi kubwa kwa wale wanaomaliza skuli bila kujifunza ujasiriamali.

(c) Je, Serikali haioni kuwa imewazidishia wanafunzi kulemaa majumbani pindi wanapomaliza skuli.

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

61. MHESHIMIWA SAADA RAMADHAN MWENDWA (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Moja ya malengo maalum ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Rais wa Kwanza wa Zanzibar Marehemu Abeid Amani Karume ni kuwapatia wananchi wanyonge makaazi bora ya kisasa hali ambayo ilipelekea kujengwa nyumba za Michenzani katika Mikoa mbali mbali.

(a) Je, Serikali bado ina nia ya kuwasaidia wanyonge hawa na ni kiasi gani wananchi hao wanatozwa kwa mwezi.

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzifanyia matengenezo nyumba hizo ambazo zimechakaa sana.

(c) Je, ni lini nyumba hizo hasa za Michenzani zilifanyiwa matengenezo makubwa kwa mara ya mwisho.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto :

109. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto

Pamoja na jitihada za serikali za kulinda haki za Wanawake, bado kuna tatizo la baadhi ya Wanawake wanapoachwa na Waume zao, kuangukiwa na mzigo wa kulea watoto peke yao kutokana na kukosa huduma za baba wa watoto hao wanaoachiwa.

(a) Je, kwa sasa Serikali ina mipango gani madhubuti ya kuwalinda wanawake wanaoachwa na watoto bila ya matunzo ya baba zao.

(b) Je, Serikali haioni kuwa sasa umefika wakati wa kupanga mikakati ya kupunguza wimbi la wajane na watoto wasiokuwa na baba ambao baadae wanakuwa mzigo kwa Serikali.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

141. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Zanzibar imezindua kituo cha kuzalisha vifaranga vya samaki.

(a) Je, tangu kuzinduliwa kituo hicho, wafugaji wangapi wamefaidika katika visiwa vya Unguja na Pemba.

(b) Je, vifaranga hivyo vinatolewa kwa wafugaji kwa utaratibu gani na mafunzo gani yanatolewa kabla ya kuingia katika ufugaji wa samaki.

(c) Je, kuna muamko kiasi gani kwa watu katika ufugaji wa samaki.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

14. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimwia Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji.

Nchi yetu inatembelewa na wageni watalii na wengine kutoka mataifa ya nje. Hata hivyo Uwanja wetu wa Ndege umekuwa na ufinyu wa nafasi. Miezi michache nyuma ndege tatu zilifika kwa wakati mmoja na kukawa misururu mirefu ya watu mpaka kwenye uwanja, hali ambayo inatia aibu nchi yetu kwa wageni hao.

(a) Kwanini miundombinu haiwekwi vizuri na kuepusha misongamano kama ile.

(b) Ni mipango gani ya dharura inafanyika kuondokana na hali ile wakati tunasubiri "terminal" mpya imalize mwaka wowote ule.

(c) Jengo la terminal II litamalizika lini ili kuondoa aibu hii tunayopata.

Wizara ya Afya:

34. MHESHIMIWA OMAR SEIF ABEID (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wagonjwa kushindwa kutoa taarifa wanapokwenda hospitali kwa kukosa huduma wanayoitegemea kutokana na kutojua ni sehemu gani inayohusika kupeleka malalamiko yao kwa watendaji ambao hawawatendei haki wagonjwa.

(a) Je, ni utaratibu gani uliowekwa wa kutoa taarifa za malalamiko kwa uongozi pale inapotokezea kwamba mfanyakazi kashindwa kuwajibika kwa mgonjwa.

(b) Je, ni utaratibu gani unaotumika kuweza kuwabaini wafanyakazi wasiowajibika ipasavyo kwa wagonjwa katika hospitali na vituo vyetu vya afya.

Wizara ya Biashara na Viwanda:

19. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Viwanda:

Baadhi ya maghala ya karafuu Tibirinzi Pemba ni matupu kama vile hayatumiki kwa ajili ya kuhifadhi karafuu.

Je, kwanini maghala hayo yapo matupu.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Ripoti ya Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018.

Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Ripoti ya Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati ya Ardhi na Mawasiliano kwa mwaka 2017/2018.

Zanzibar,
01 Oktoba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.